

## **HALMASHAURI YA MANISPAA YA LINDI**

### **UDHIBITI UVUVI HARAMU NA UTOROSHAJI WA MAZAO YA BAHARI NJE YA NCHI**

#### **UTANGULIZI**

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi ina mwambao wa bahari usiopungua wastani wa urefu wa km. 112 kutoka Mtaa wa Mkwaya kata ya Mingoyo kusini hadi mtaa wa Likong'o kata ya Mbaja Kaskazini mwa Manispaa. Ukanda huu wa Bahari una fukwe nyingi zinazofaa kwa shughuli za uvuvi, ufugaji wa viumbe vyta majini kama vile Samaki, Kaa, Chaza na kilimo cha Mwani. Jamii ya wakazi waishio katika Mwambao huo, zaidi hutegemea uvuvi katika kujikimu kimaisha, wavuvi hao hutumia zana/ teknolojia ya vyombo duni ambavyo huwalazimisha kuvua karibu na pwani Vyombo hivyo ni ngalawa , mashua, madau, na mitumbwi na baadhi yao ni wale waendao kwa miguu .

#### **HALI YA UVUVI**

Hali ya uvuvi kwa Halmashauri ya Manispaa ni ya wastani kutokana na vyombo duni ambavyo vinatumwa na wadau walio wengi katika shughuli za uvuvi visivyoendana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Wavuvi wengi hutumia ngalawa na mitumbwi ambayo haitumii mashine za kuwawezesha kufika mbali, hali hii inasababisha idadi kubwa ya wavuvi kuvua kandokando mwa fukwe kwa kutumia nyavi zenyenye matundu madogo (kokoro) na wengine kutumia vilipuzi kama vile baruti katika shughuli za uvuvi.

Halmashauri ya Manispaa ya Lindi katika kutekeleza agizo la Mheshimiwa Rais Dr. John Pombe Magufuli alilotoa tarehe 11 Agost, 2016 huko jijiji Mwanza la kuthibiti uvuvi haramu imefanya yafuatayo ili kuhakikisha uvuvi unakuwa endelevu kwa vizazi vyta sasa na vijavyo;

1. Kuandaa mpango mkakati wa kuthibiti uvuvi haramu ambaa umeainisha shughuli mbalimbali zitakazofanyika ili kutokomeza uvuvi haramu. Mpango huo kwa sasa ndio unaotumika kama dira katika kuthibiti uvuvi haramu katika Manispaa ya Lindi. Mpango mkakati huo umeambatanishwa pamoja na ripoti hii.

2. Kutoa matangazo kwa vipasa sauti na katika mbao za matangazo juu ya uvuvi haramu kwenye mialo na makambi 14 ambapo shughuli za uvuvi hufanyika.
3. Kubandika matangazo yenyenje ujumbe juu ya uvuvi haramu kwenye mialo na makambi ya wavuvi na kuwataka kusalimisha zana za uvuvi haramu (nyavyu zenye matundu madogo (kokoro), vilipuzi nk) kwa Mwenyekiti wa Mtaa au Mtendaji wa Mtaa au Kata ambapo nyavyu zenye matundu madogo (kokoro) (17) zenye urefu wa mita 480 zilisalimishwa.
4. Kufanya mikutano na vikundi 16 vya wavuvi pamoja na wananchi kwa ujumla kutoka mitaa ya Mbanja, Mitwero, Benki, Mingoyo, Ufukoni, Mikumbi, Kitumbikwela Uganda na Tulieni na kuwaelimisha madhara ya uvuvi haramu. Katika mikutano hiyo wavuvi waliahidi kutoshiriki katika shughuli za uvuvi haramu. Baada ya mikutano wananchi wamekuwa na hamasa kubwa ya kudhibiti uvuvi haramu kwa baadhi ya maeneo kama Mwitingi na Mbanja ambapo wameshiriki kikamilifu na kuwa msitari wa mbele katika kukomesha uvuvi haramu.
5. Doria 10 zimefanyika katika bahari kuu na fukwe za bahari kwenye maeneo ya mikoko kwa ajili ya kudhibiti uvuvi haramu pamoja na kufuatilia wavuvi ambao hawajasajiliwa ambapo tulifanikiwa kukamata kokoro 4 na wavuvi 4 ambao walikuwa wanavua kwa kutumia mabomu na mvuvi mmoja alikuwa anatumia sumu. Wavuvi hao (4) walikamatwa wote na kupelekwa mahakamani wakiwa na vilipuzi na huyo mmoja aliyekuwa anatumia sumu alikamatwa akiwa na samaki waliodhaniwa kuvuliwa kwa sumu naye alifikishwa polisi kwa hatua za kisheria.
6. Kamati ya ulinzi na usalama ya mkoa kwa kushirikiana na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya pamoja na Manispaa ilifanya doria ukanda wa pwani na bahari kuu ikishirikiana na kamati ya doria kanda ya kusini (marine police) ili kuongeza nguvu katika kidhibithi uvuvi haramu. Doria hii ilifanyika ukanda wote wa pwani kuanzia Mtwara hadi Kilwa. Kwenye Manispaa yetu ya Lindi kamati hii ilifanikiwa kukamata chombo kimoja cha uvuvi kutoka Zanzibar chenye namba za usajili WMJU 1244 kikiwa na wavuvi 8 waliokuwa wakielekea nchini Msumbiji lakini hawakuwa na leseni za uvuvi hivyo wakalazimika kukata leseni za ndani ya Manispaa ya Lindi kabla ya kuendelea na safari. Vivuli (photocopy) za leseni zao ziliwasilishwa polisi kitengo cha upeletezi kama uthibitisho wa kuwa wavuvi hao wamekata

leseni na wameruhusiwa kuendelea na safari yao, vilevile kamati ilifanikiwa kukamata kokoro 3, mikuki 4, vioo 3 na magamba 18 ya kasa ambao hawaruhusiwi kuvuliwa na watuhumiwa 2 ambao walifkishwa polisi kwa hatua za kisheria.

7. Kufanya ukaguzi wa mazao ya bahari katika mnada wa soko kuu la samaki na stendi ya Mkoa ili kuhakikisha samaki wanaouzwa hawajavuliwa kwa uvuvi haramu.
8. Halmashauri imeendelea kuvisimamia vikundi 13 vilivyowezeshwa zana bora za uvuvi kupitia WAMA, MACEMP na TASAF ili kuendelea kuajiri wavuvi wengi na kuwatoa katika uvuvi haramu. Pia wavuvi hao hutumika kutoa elimu ya athari za uvuvi haramu kwa wavuvi wengine.
9. Kwa ushirikiano wa BMUs, Watendaji wa Kata, Mitaa pamoja na Wenyeviti wa serikali za mitaa tulikusanya majina ya wavuvi wanaotuhumiwa kujihusisha na uvuvi haramu ambapo wavuvi 22 wanajihuisha na uvuvi kwa kutumia baruti (vilipuzi) na sumu, na wavuvi 95 wanaojihuisha na shughuli za uvuvi kwa kutumia nyavye zenye matundu madogo (kokoro) majina ya wavuvi hao yaliwasilishwa kwenye kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya kwa ajili ya uchunguzi. Majina hayo yameambatanishwa katika taarifa hii kama inavyooneshwa kwenye orodha ifuatayo;

**A: MAJINA YA WAVUVI WANAOJIHUSISHA NA UVUVI HARAMU KWA KUTUMIA VILIPUZI (BARUTI)**

**B: MAJINA YA WAVUVI WANAOJIHUSISHA NA UVUVI HARAMU KWA KUTUMIA KOKORO**

**C: MAJINA WA WAVUVI WALIOSALIMISHA ZANA ZA UVUVI HARAMU (KOKORO)**

SN	JINA	KATA	MTAA
1	Mohamedi Mtoro	Msinjahili	Tankini
2	Yusufu Saburi	Msinjahili	Mlandege

3	Ahamedi Ally Mkanjope	Msinjahili	Mlandege
4	Issa Salumu Nalinga	Msinjahili	Kanisa
5	Selemani Khalfani Mbwana	Msinjahili	Kanisa
6	Musa Mohamedi Mmbwa	Msinjahili	Kanisa
7	Bakari Yusufu Mpanjile	Rasbura	Zahanati
8	Ahamadi Selemani	Rasbura	Mitweto stand

10. Halmashauri ya Manispaa ya Lindi kwa kushirikiana na kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ilifanya mukutano na wavuvi wote waliotuhumiwa kuhusika na shughuli za uvuvi haramu na kuwaeleza madhara ya uvuvi haramu katika mazingira ya bahari na viumbe wake ambapo wavuvi waliahidi kuachana na uvuvi haramu.

## HITIMISHO

Kwa sasa hali ya uvuvi haramu katika Halmashauri ya Manispaa ya Lindi imepungua kiasi kutokana na kufanya doria za mara kwa mara, kuwatoza *fine* wavuvi wanaokiuka sheria ya uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009.

Kwa sasa Halmashauri inaendelea kutumia sheria zake ndogo katika kudhibiti vitendo vyta uvuvi haramu, kushirikiana na kamati za ulinzi shirikishi za rasilimali za bahari (BMU), Wenyelevi wa serikali za mitaa pamoja na wanachi kuhakikisha kuwa rasilimali za bahari zinalindwa kikamilifu. Aidha Wananchi kwa sasa wamekuwa mstari wa mbele katika kutoa taarifa juu ya uvuvi haramu pamoja na kuwakamata wavuvi wanaojihusisha na uvuvi haramua na kuwfikisha polisi.

Tatizo lililopo katika kipindi hiki katika Manispaa ya Lindi ni wavuvi wadogowadogo ambao wanavua kwa kutumia nyavy za matundu madogo (kokoro) katika maeneo ya fukwe, ingawa wataalam wakishirikiana na viongozi wengine wameendelea kuwadhibiti kwa doria mbalimbali.